102/3

**FASIHI YA KISWAHILI**
KARATASI YA TATU

**Julai / Agosti 2016**

Muda: Saa 2½

# MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA WESTLANDS

## Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
**Kidato cha Nne**

## FASIHI YA KISWAHILI
Karatasi - 102/3
**Julai / Agosti 2016**
**Muda :** Saa 2½

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**MAAGIZO**

- Jibu maswali **MANNE** pekee.
- Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**.
- Kisha chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizobakia; yaani Riwaya, Tamthilia, Fasihi Simulizi na Ushairi.
- Usijibu maswali **MAWILI** kutoka **SEHEMU MOJA.**
- Kila swali lina alama 20.
- Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
- Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.
- Watahiniwa wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. **(LAZIMA)**
**SEHEMU A: HADITHI FUPI**
**Damu Nyeusi na Hadithi nyingine** : ***K. Walibora na S.A. Mohamed***

"Jitihada haiondoi kudura." Huku ukirejelea hadithi zozote **tano** katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi nyingine*, eleza ukweli wa methali hii. (alama 20)

**SEHEMU B : RIWAYA:**
**Kidagaa Kimemwozea ; *K. Walibora***
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "Unautukanisha ukoo wetu mtukufu. Siku hizi hata naona aibu kukuita ndugu yangu".

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Wahusika hawa ni riale kwa ya pili? Fafanua. (alama 16)

**AU**

3. Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* imeangazia kwa kina ujenzi wa jamii mpya. Thibitisha kwa kurejelea mifano **kumi**. (alama 20)

**SEHEMU C : TAMTHILIA**
**Mstahiki Meya : *Timothy M. Arege***
**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Nina hakika umeona mji ulivyo mchafu. Harufu kila mahali . . ."

a) Eleza muktadha wa usemi huu. (alama 4)

b) Fafanua sifa **nne** za msemewa. (alama 4)

c) Kwa kutoa mfano taja mbinu moja ya sanaa inayojitokeza katika dondoo. (alama 2)

d) Mbali na harufu inayorejelewa katika dondoo hili, jadili 'harufu' nyingine inayojitokeza katika baraza la mji wa Cheneo. (alama 10)

**AU**

5. a) Kwa kurejelea Tamthilia ya *Mstahiki Meya* eleza matumizi ya : (alama 10)

i) majazi

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

ii) uzungumzi nafsia

iii)nyimbo / ushairi

iv)tashbihi

v) kuchanganya ndimi

b) "Siuoni mpango wa kuwanufaisha watu wetu."

i) Msemaji analalamikia manuafaa gani katika muktadha huu? (alama 4)

ii) Eleza umuhimu wa msemaji. (alama 6)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

**6.** a) i) Kwa kutoa mfano mmoja eleza dhana ya maigizo. (alama 2)

ii) Fafanua dhima ya maigizo. (alama 8)

b) Nafasi ya miviga katika jamii ni muhimu. Jadili aina **tano** zozote za miviga. (alama 10)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU E: USHAIRI**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Sebuleni niliketi
Mapema moja jioni
Nikaanza kumbo kuupiga
Mlima wa ugali

Mboga na nyama nikautowelea
Kabla ya maziwa mafunda kupiga
Na maji kuteremsha, koo kusafisha

Pembeni niliketi
Nikipumua kwa shida
Na kushindwa kujinyanyua
Taratibu askari wakaninyemelea
Na bakunja kunipiga

Nilipozinduka nilikuta changu kisanduku
Macho kikiwa, habari kinamwaya
Ndipo nikaona wenzangu wananchi
Mizizi wakila na matunda mwitu
Vyote wakivisaka kwa taabu

Katika mazingira hayo ya sarabi
Miili yao ilikuwa taabu kuibeba
Kwa unyonge wa njaa.

Nikashangaa tulivyoishi
Chini ya bendera moja
Lakini tukiwa mbalimbali
Katika limwengu tofauti

Kama ardhi na mbingu

a) Eleza aina ya shairi hili? (alama 2)

b) Tambua nafsineni katika shairi? (alama 2)

c) Fafanua sifa za utunzi alizotumia mshairi. (alama 4)

d) Eleza toni ya mshairi inayojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa pili. (alama 2)

e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 5)

f) Kwa kurejelea shairi dondoa mifano **miwili** ya mbinu za lugha. (alama 2)

g) Fafanua maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

i) kumbo

ii) bakunja

iii)sarabi.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com